www.xtrapapers.com



Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili A: literature – Standard level – Paper 1
# Swahili A : littérature – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili A: literatura – Nivel medio – Prueba 1

Friday 8 May 2015 (afternoon)
Vendredi 8 mai 2015 (après-midi)
Viernes 8 de mayo de 2015 (tarde)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

## Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a guided literary analysis on one passage only. In your answer you must address both of the guiding questions provided.
- The maximum mark for this examination paper is **[20 marks]**.

## Instructions destinées aux candidats

- N’ouvrez pas cette épreuve avant d’y être autorisé(e).
- Rédigez une analyse littéraire dirigée d’un seul des passages. Les deux questions d’orientation fournies doivent être traitées dans votre réponse.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d’examen est de **[20 points]**.

## Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un análisis literario guiado sobre un solo pasaje. Debe abordar las dos preguntas de orientación en su respuesta.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[20 puntos]**.

2215–0199

5 pages/páginas

© International Baccalaureate Organization 2015

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

www.xtrapapers.com



Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi. Ni lazima kuzingatia maswali mawili uliyotolewa kama mwongozo kwenye jibu lako.

**1.**

Baada ya kimya kirefu aliongeza “Hujui! Hujui Hasara! Hujui kama wewe ni punda tu ambaye amezaliwa kwa ajili ya kuwatumikia wengine. Hujui kama wewe ni kasuku tu uliyeumbwa ili kuwastarehesha wengine. Hapo ulipo una nini cha thamani? Una raha gani ya kuishi duniani? Tazama unavyolala kwa dhiki kuliko hata mbwa wao,” alisita kwa muda. Alipoanza tena kuongea sauti yake ilikuwa na upole zaidi.

“Hasara, rafiki yangu. Tumekuwa pamoja tangu utotoni. Tumewalamba miguu tangu utotoni. Sasa tunaendelea uzeeni. Wanataka tuendelee kuwalamba miguu tangu utotoni. Sasa tunaelekea uzeeni. Wanataka tuendelee kuwalamba miguu hadi kaburini. Wana hila zote za kufanya tushindwe kutoka katika bwawa hili lenye matope yaliyotunasa viunoni, ili tuendelee kuwalamba miguu. Juhudi zetu zote za kujikwamua wanazivuruga na kutudhihaki. Unakumbuka nilikwambia nini utotoni Hasira? Kwamba ‘nitafanya kila mbinu kujitoa katika utamaduni huu wa umaskini’ na nimefanya kila kitu. Nimejaribu kuishi kama wao na kuthubutu kufuata mbinu zao. Hawataki. Nimeamua kutumia hila zao. Bado hawataki. Ni nini wanachotaka? Ninunue bastola na kuvamia benki zao ili wanifunge maisha au waninyonge?”

Alisita tena, “wao wanafanya kila kitu. Wanapeana mikopo kwa mamilioni, mikopo ambayo hailipwi. Wanapeana mbinu za kuimbia serikali na mashirika yake usiku na mchana; mbinu ambazo haziingiliwi. Wanapeana nafasi zote za kujielimisha; elimu ambayo sisi haitusaidii. Wanapeana matibabu ya maana, siye tunakufa kama mifugo. Wanapeana vibali vyote vya biashara za maana; siye tunaishi kuwa vibarua wao.”

“Hawataki tufanye lolote,” alifoka ghafla. “Hawataki. Hawataki kabisa,” mara alitabasamu. Lilikuwa tabasamu linalotisha kuliko macho yake, “Jambo la kushangaza ni kwamba pamoja na kwamba hawataki tuishi bado hawataki tufe vilevile. Wanataka tuendelee kuishi. Unajua ni kwa nini? Wanataka tuishi ili tuendelee kuwatumikia,” akasita. Taratibu, akalisahau kochi hilo bovu na kujikuta akilalia kitanda chenye godoro gumu la pamba. Kando ya Hasira.

“Sikia rafiki yangu Hasira. Kitu kimoja lazima waelewe. Maisha yetu yana thamani kama yao. Hilo lazima waelewe. Watake wasitake. Badala ya kutufundisha kupigania maisha yetu hapa, wanatupeleka nje ya nchi kupigania watu wengine. Wengi wetu hatuelewi. Wewe na mimi tunaelewa. Tumetoka mbali. Tunajua wenyewe tulikotoka. Hivyo hatutalala usingizi hadi tutakaposhinda.”

Akacheka tena. Safari hii kilikuwa kicheko halisi. Kicheko cha kibinadamu. Tofauti kabisa na kile cha kishetani ambacho kilikuwa kikicheza katika macho yake kama sumu. “Niwie radhi Hasara. Damu ilichemka kidogo.” Sio mchezo kupoteza milioni ishirini ambayo ilikuwa ikinukia kabisa mikononi na juu yake kupata hasara ya laki tatu. Usijali. Kwa ufupi ni kwamba nilikuwa nikifanya mpango wa biashara ndogo ya ujanja ujanja kama wanavyotaka wao. Nilitaka mara baada ya kuichukua pesa ile nimuue yule Bwana. Kwani yeye si mtu wa kuimbiwa milioni ishirini na kunyamaza. Angetumia kila mbinu na kunipata. Na kama asingepata pesa zake angeichukua roho yangu badala yake. Hivyo kifo chake kingekuwa uhai wangu.

“Sasa sikia. Safari hii wameshinda. Kwa kweli nilikuja hapa kukuambia kuwa hakuna haja tena kumuua yule Bwana. Mwache. Hata hivyo siku mbili tatu baadaye nitakuona kwa jambo muhimu zaidi. Ikibidi nitaleta hata bastola ili ujifunze kuitumia,” akainuka na kuelekea mlangoni. “Utaogopa kutumia bastola Hasara, wakati risasi moja tu itakuwezesha kumiliki milioni ishirini?”

Bila ya kusubiri jibu la Hasara, aligeuka na kutoka nje. Muda mfupi baadaye mngurumo wa gari yake ulisikika na kutokomea.

www.xtrapapers.com



45 Sasa! Hasara aliwaza akicheka peke yake. Hasira naye anahubiri siasa! Mwanasiasa ahubiri siasa. Mwananchi wa kawaida ahubiri siasa hiyo siasa ni kitu gani? Fimbo ya kujipigia watu au ngao ya kujikinga?

Ben R Mtobwa, *Dar es Salaam Usiku* (1998)

(a) Mwandishi ameweza kutumia mtindo kwa njia gani ili aweze kupitisha ujumbe wake?

(b) Jadili maudhui muhimu yanayojitokeza katika makala haya na yanvyoathiriwa na ploti ya mwandishi.

www.xtrapapers.com



**2.**

**Dunia**

Dunia yayumbayumba, kama wimbi la bahari
Dunia ni kama jumba, la anasa furi furi
Dunia itakufumba, ukosapo tahadhari
Dunia kama bahari, hadhari itakutosa.

Dunia kwa mtazamo, ina umbo la mkonge
Dunia wema haumo, tahadhari sikukenge
Dunia uwi u mumo, wenye mithili ya nge
Dunia ni msumeno, yakata mbele na nyuma.

Dunia kimulimuli, yajipamba kwa uzuri
Dunia taka akili, mja kuitafakari
Dunia bila akili, itakutia kabari
Dunia kitendawili, huenda ikatutanza.

Dunia sikumbatile, ukaifanya rafiki
Dunia sing’ang’anile, ukaiga halaiki
Dunia siegemele, dunia siidhihaki
Dunia mti mkavu, mwanadamu silemele.

Dunia umbo duara, siifanyie makeke
Dunia kama mpira, huijui mwanzo wake
Dunia ina hasara, enye waume kwa wake
Dunia kigeugeu, ina muigo wa lumbwi.

Dunia kiichezea, itakutia skuli
Dunia takuzomea, hata ukiwa rijali
Dunia haitanywea, au wifanye dhalili
Dunia ni kama mwamba, vishindo kuvihimili.

Dunia sio maguvu, nakuonya anfari
Dunia kwa wasikivu, mambo huwendea shwari
Dunia sio lemavu, kueza kuihasiri
Dunia ni kama mavu, mjuzi wa kuhasiri.

Dunia haina wema, imechagua ushari
Dunia si kama mama, mwenye malezi mazuri
Dunia itakutema ukosapo tahadhari
Dunia ni ya waume, kanyaga kwa tahadhari.

Dunia yakuhadaa, kukuonesha uzuri
Dunia ina balaa, ichungue kwa uzuri
Dunia ukiivaa, utaona yake shari
Dunia ni mchongama, upande kwa tahadhari.

Timothy Arege, *Tunu ya ushairi* (2013)

www.xtrapapers.com



(a) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili?

(b) Jadili kuhusu matumizi ya mtindo na muundo katika shairi.